


Gharama Haramu



Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa
kushirikiana na Twaweza.

Waandishi:
Richard Mabala na Churchill Shakim

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Justice Rutenge na Evarist Kamwaga, Twaweza

Usanifu:
Churchill Shakim

©Tamasha/Twaweza - 2013



Barua:
TAMASHA
S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255-714-661-544
Baruapepe: vtamasha@gmail.com
general@tamashavijana.org
Wavuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa
sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni
kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili nakutuma nakala
mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Wapendwa wasomaji,

Maji yasiyo salama ni chanzo kikubwa cha magonjwa ya kuhara na mengineyo. Ndiyo maana ni muhimu kupata maji kutoka kwenye vyanzo vilivyoboreshwa. Hivi ni vyanzo ambavyo haviruhusu uchafu kutoka nje kuingia kwenye maji yetu kama vile mabomba au visima vilivyofunikwa. Je, ni jukumu la nani kuhakikisha kwamba tunapata maji yetu kutoka kwenye vyanzo bora? Je, tunafanya nini kama mabomba yetu hayatiririshi maji? Tutakaa muda gani kuwasubiri wengine kutuletea maji salama?

Fuatilia hadithi hii kujua wengine walifanya nini.

Richard Mabala
Mkurugenzi, TAMASHA

Wahusika



Bonge

Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo
na mkereketwa wa maendeleo



Bibiye

Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati




Mwenyekiti

Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda
maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje
kuliko nguvu ya wananchi



Mtendaji

Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma
yao ya kuchukua hatua wenyewe





Lakini wewe Bonge,
mbona maji yako ni
machafu hivyo?

Yaani mama
hujui. Kile kisima
ndivyo kilivyo.
Tunashindana na
wanyama.

Kufuru
kabisa!

Lakini kwanini tusichangie
kutengeneza pampu? Mambo
yote yangeisha.

Aka, mwemzangu. Pampu
hii ni ya wafadhili.
Wafanye kazi yao.



Na kipindupindu pia
kitakuwa cha mfadhili?
Ni kazi yetu.

Waambie watu
wa kamati ya
maji basi.

Lakini kazi yako kutafuna
pesa zetu.

Una uhakika?
Na kama wajua
umechukua
hatua gani?




Wanaenda kwa Mwenekiti

Mnalalamika nini?
Pampu ikiharibika si
mnapata biashara
nzuri zaidi.


Kweli mwenyekiti
wasema hivi?
Wananchi wanapata
shida.





Sikiliza Bonge, mimi
sina riguru. Kisima
cha mfadhili, pampu
ya mfadhili, ni kazi
yake kutengeneza.


Si kweli.
Kwa sera ya maji
ni kazi yetu.



Usiniletee siasa zako
bwana. Nikiwaambia
wananchi wachangie
watanimeza mzimanzima.

Hivi kazi ya kiongozi
ni kuogopa au kuongeza?





Kwa nini umepandisha
bei hivyo?

Wewe mama kule
mbali. Na barabara mbovu.
Tukienda mbali zaidi, lazima
tupandishe bei.

Visingizio tu. Pampu
ikiharibika mnataka
kufaidi ninyi tu.




Lakini nimewaambia
tuchangie tutengeneze.

Usituletee upumbavu
wako hapa. Watutesa
kisha wataka tuchangie
tena.









Anaingia Bibie


Bonge umenisikitisha
sana. Umetusaliti
namna hiyo?

Hujui usemalo.
Tunajisaliti
wenyewe kwa
kutotaka kuchukua
hatua.



Lakini si kazi
yetu. Lazima
Serikali
iwajibike.





Wewe ni mwelimishaji
rika. Ukikuta serikali
haijafanya kitu utanyamaza
tu? Mabadiliko ni wewe...
Lazima ufanye kitu.

Nakubali. Lakini sitatumia
nafasi yangu kuwanyonya
watu kama wewe
unavyofanya.

Fungua
Bwana tupate
majji!


Kwani hamjasikia?
Bonge kakimbia.
Kachuma pesa,
kaondoka jana usiku
na wenzake wawili.




Hawa vijana lazima wachukuliwe
hatua. Ni wapinzani, ni wahaini,
wanatumia shida zetu kujinufaisha
wenyewe na kupanya sisi
tuonekane wabaya.



Mwenyekiti, nadhani siyo
haki kutuhukumu bila
kutusikiliza.





Tulisema mchange,
hamkutaka. Tulinwambia
mwenyekiti hebu
tuchange kulingana na
sera ya taifa, hakutaka,
basi tumefanya wenyewe.

Mabadiliko ni sisi
bwana.

Kipuri hiki shilingi laki moja
tu, yaani sanasana ni ndoo
elfu mbili. Kwa kuwa hamkuwa
tayari kuchangia, tulipandisha
bei kwa siku kumi tu pesa
zilitosha.





Lakini wewe rawe.
Hata kuniambia nimi
mwaraharakati
mwenzio.



Nilitaka wote mwiipate.
Baada ya uchungu
mtaacha kuchonga.





Bonge

Hamjambo, wasomaji wetu

Tunadhani sasa mmetusoma sana, mapambano yetu, makosa yetu na mafanikio yetu.

Ni matumaini yetu kwamba mmefurahia jitihada zetu za kuboresha maisha ya watu.

Lakini lazima mjue kwamba sisi sio viongozi.

Sisi ni watu wa kawaida kama ninyi.

Tunahangaika kutafuta maisha. Tunalia kutoboka kwa mifuko yetu.

Tunakereka mambo yasipoenda sawa.

Tuna tofauti moja tu na watu wengi.

Tukikereka hatuishii kulalamika, tunachukua hatua.

Mabadiliko ni sisi.

Ndiyo maana tumewaletea vijitabu hivi kuwaonyesha kwamba mabadiliko yanapatikana tukiyapigania sisi wenyewe.

Hebu jaribuni na ninyi ili tupate mifano yenu. Mtashangaa!

Tujiunge sote kuboresha maisha ya wote.

Je wajua?

- Vyanzo vya maji kijijini vinapaswa kusimamiwa na vikundi huru vya watumia maji, sio tena kamati za maji kama ilivyokuwa.
- Vikundi hivi vina jukumu la kukusanya na kutunza fedha kutoka kwa watumia maji na kuzitumia kuendesha vyanzo vya maji.
- Endapo chanzo cha maji kimeharibika, kikundi cha watumia maji kina wajibu wa kufanya matengenezo, ikiwa ni pamoja na kununua vipuri, kugharamia ufundi na kulipia matengenezo.
- Vikundi hivi vinapaswa kutambuliwa na Serikali ya kijiji na kusajiliwa kwenye Halmashauri ya wilaya ili vitambulike kisheria na kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa.



Tufanyeje?

- Tuache kuwa wategemezi. Utegemezi ni aiibu.
- Sisi ndio wamiliki wa maji yetu, kwa utaratibu maalum. Si Serikali wala kamati za maji za vijiji. Tuunde vikundi vyetu vya watumiaji wa maji na kuchagua viongozi wake sisi wenyewe, kisha tuweke utaratibu wa kusimamia mapato na matumizi vizuri.
- Tusikubali kuteseka kutokana na kuwangoja wengine watengeneze. Mabadiliko ni sisi.
- Tuchangamke. Tuunde vyombo vyetu na kuvisimamia imara.

TUKIAMUA TUTAJIKWAMUA

Je, umewahi kufanya jambo lolote la kishujaa kama Bonge na Bibie?

Au unamfahamu mtu mwingine aliyefanya kitu cha kipekee kuisaidia jamii yake?

Kama jibu ni ndiyo, tungependa utusimulie!

Tafadhali tutumie hiyo stori yako iliyoleta mabadiliko hapo unapoishi au iliyotokea mahali pengine.

Tunaweza kuitumia stori yako kuandaa vijitabu au vipindi vya Televisheni na redio ili kuelimisha wengine. Usikose kutumia fursa hii!

Anuani:

Barua: Twaweza-Shujaa, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua-pepe: shujaa@twaweza.org

Simu: Tuma ujumbe mfupi (SMS) bure ukijumuisha neno SHUJAA kwenda **namba 15381**